washington
healthplanfinder
click. compare. covered.

Fasili za Maneno Muhimu ya Bima ya Afya

# Maneno Muhimu ya Mwongozo wa Mtumiaji



MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Makato

## MAKATO NI NINI?

Makato yako ni kiasi unachopaswa kulipia matibabu kabla ya bima yako kuanza kushiriki gharama. Kiasi cha makato yako kinaanza upya mwanzoni mwa kila mwaka.

## MFANO

Marcus na makato ya $2,000. Analazwa hospitali na inagharimu $10,000. Marcus lazima alipe makato yake kabla ya bima yake ya afya kulipia gharama zozote zile. *(Makato na gharama nyingine zinatofautiana kati ya bima za afya.)*

**$8,000**

Sehemu inalipwa na bima yake ya afya

**$2,000**

Makato yanalipwa na Marcus

**$10,000**

Kulazwa hospitali



MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Orodha ya Dawa

## ORODHA YA DAWA NI NINI?

Orodha ya dawa ni dawa zinazojumishwa kwenye bima yako ya afya. Bima yako ya afya italipia sehemu au gharama zote za dawa hizi.

## MFANO

George anakwenda duka la dawa muhimu kununua dawa alizoandikiwa. George anampa mfamasia orodha yake ya dawa. Bima yake ya afya italipia dawa. George analipa tu malipo yake shirikishi ya $20. Bima yake inalipia gharama iliyosalia. *(Kiasi cha malipo shirikishi kinatofautiana kati ya bima za afya)*



**$20**

kwa kila dawa

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Mtoa Huduma za Afya Mkuu

## MTOA HUDUMA ZA AFYA MKUU NI NANI?

Mtoa Huduma za Afya Mkuu ni daktari au muuguzi mkuu unayemwona kama sehemu ya bima yako ya afya. Mtoa huduma za afya mkuu anasimamia matibabu yako. Anaweza kushirikiana na mtaalamu kuhakikisha una afya njema.

## MFANO

Hapo awali, Roger alienda Chumba cha Matibabu ya Dharura alipojisikia mgonjwa. Kwa sasa, ana bima ya afya inayomwezesha kuchagua mtoa huduma za afya mkuu. Akijisikia mgonjwa, anamtembelea mtoa huduma za afya mkuu, naye anaweza kumtibu ugonjwa wake. Roger akihitaji matibabu maalum, mtoa huduma za afya mkuu atamuunganisha na mtaalamu.



Mtembelee mtoa huduma wako wa msingi kwa ajili ya uchunguzi, uangalizi usiokuwa wa dharura na uangalizi wa mtandaoni.

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Fedha za Malipo ya Bima


## FEDHA ZA MALIPO YA BIMA NI NINI?

Fedha za malipo ya bima zinashusha kiasi unacholipa kwa ajili ya bima yako ya afya kila mwezi. Kiasi cha fedha za bima unachopata kinategemea na kipato chako.

Tembelea **wahealthplanfinder.org** au piga **1-855-923-4633** kwa taarifa zaidi

## MFANO

Marcela ni mtu mzima mseja asiye na bima ya afya. Kipato chake cha mwaka ni $25,000. Anapata fedha za bima kwa sababu ya ngazi ya kipato chake. Marcela anaweza kutumia fedha hizi kushusha malipo yake ya kila mwezi. *(Kiasi halisi kinatofautiana.)*



Gharama ya malipo ya bima − Fedha za malipo ya bima = Malipo ya chini ya kila mwezi

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Bima Shirikishi

## BIMA SHIRIKISHI NI NINI?

Bima Shirikishi ni sehemu yako ya gharama ya huduma inayolipiwa na bima ya afya. Utaanza kulipa bima shirikishi baada ya kulipia makato ya bima yako ya afya. Bima shirikishi ni moja ya njia utakazoshiriki gharama ya huduma yako ya afya kupitia bima yako.

## MFANO

James amelipa makato yake. Amepewa bili ya $500 kwa kumwona daktari. James analipa 20% ya bili, au $100. Bima yake ya afya italipia gharama inayosalia. *(Kiasi cha bima shirikishi kinatofautiana kati ya bima za afya.)*



**%20** Bima shirikishi 20%

x

**$500** Jumla ya bili $500

---

**$100** James anapaswa kulipa $100

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Ada ya Bima

## ADA YA BIMA NI NINI?

Ada ya bima ni kiasi unacholipa kila mwezi kwa ajili ya bima yako ya afya. Unapaswa kulipia ada yako ya bima hata kama hupokei huduma zozote za afya. Wasiliana na kampuni yako ya bima ukiwa na maswali yoyote ya malipo.

## MFANO

Jean analipa ada yake ya bima ya afya kila mwezi, kama bili ya simu yake. Jean anatuma malipo yake kwa njia ya posta siku chache kabla au analipa mtandaoni ili kuhakikisha malipo yake yanafika kwa wakati.




Hakikisha unatuma mapema malipo yanayotumwa kwa njia ya posta.

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Kutoka Mfukoni

## KUTOKA MFUKONI NI NINI?

Gharama za kutoka mfukoni ni kile unacholipa kwa ajili ya huduma za afya. Zinajumuisha makato, bima shirikishi na malipo shirikishi. Kiasi chochote kisichojumuishwa kwenye bima yako ni gharama ya kutoka mfukoni.

## MFANO

Shirley ana watoto wawili. Analipa malipo shirikishi ya $20 kila wakati yeye au watoto wake wanapomwona daktari. Familia yake itamwona daktari mara 15 katika mwaka huu. Gharama kutoka mfukoni ya Shirley itakuwa $300. *(Kiasi hiki ni cha makadirio. Piga simu kwa kampuni yako ya bima kwa taarifa zaidi.)*



**$20** kila akimwona daktari

x **15** Kumwona daktari mara 15

---

**$300** kwa mwaka

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Mtandao

## MTANDAO NI NINI?

Mtandao ni orodha ya watoa huduma wanaokubaliwa na bima yako ya afya. Watoa huduma wa ndani ya mtandao wanaidhinishwa na bima yako ya afya. Watoa huduma wa nje ya mtandao hawaidhinishwi na bima yako ya afya. Utalipa zaidi kwa huduma kutoka kwa watoa huduma wa nje ya mtandao.

## MFANO

Laura anataka kumwona mshauri wa afya ya akili. Anampata mmoja karibu na anapoishi. Kabla ya kuweka miadi, anahakikisha mtot huduma huyo yupo ndani ya mtandao wa bima yake. Itamgharimu Laura zaidi ikiwa atachagua mshauri wa nje ya mtandao.




Uliza kama mtoa huduma yupo ndani ya mtandao kabla ya kuweka miadi.

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Malipo Shirikishi

## MALIPO SHIRIKISHI NI NINI?

Malipo shirikishi ni kiasi unacholipa kwa ajili ya huduma ya afya inayolipiwa na bima yako. Huduma kama kumwona daktari au kununua dawa za kuandikiwa zitakuwa na malipo shirikishi. Malipo shirikishi yanapaswa kulipwa unapopokea huduma.

## MFANO

Thomas ana shinikizo la juu la damu. Anamwona mtoa huduma wake mkuu kila baada ya miezi mitatu. Bima yake ya afya inahitaji malipo shirikishi ya $20 kwa kumwona daktari. Thomas anamlipa daktari malipo shirikishi kila anapomwona. *(Kiasi cha malipo shirikishi kinatofautiana kati ya bima za afya.)*



**$20**

kila akimwona daktari

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Huduma za Kinga

## HUDUMA ZA KINGA NI NINI?

Huduma za kinga zinalipiwa na bima yako ya afya huku wewe ukilipia gharama kidogo sana au kutolipa kabisa. Zinajumuisha uchunguzi na sindano za mafua kila mwaka. Huduma hizi zinalipiwa tu ukimwona mtoa huduma wa ndani ya mtandao.

## MFANO

Taylor anafanyiwa uchunguzi na sindano ya mafua ili awe na afya njema. Taylor anafurahia kwamba bima yake ya afya inalipia huduma zinazomkinga asiumwe.



Huduma za kinga zinakusaidia kuwa mwenye afya njema.

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Mafao Muhimu ya Kiafya

## MAFAO MUHIMU YA KIAFYA NI NINI?

Mafao muhimu ya kiafya ni seti ya huduma za afya ambazo zinalipiwa na bima zote. Baadhi ni bure. Baadhi zina malipo shirikishi au bima shirikishi.

Mafao muhimu ya kiafya yanajumuisha:

- Kumwona daktari na kulazwa hospitali
- Kutembelea chumba cha wagonjwa mahututi (emergency room)
- Uangalizi kabla na baada ya mtoto kuzaliwa
- Huduma za matibabu ya afya ya akili na matumizi ya dawa za kulevya
- Dawa za kuandikiwa na daktari
- Huduma na vifaa vya kukusaidia kupona ikiwa umeumia au una ulemavu au ugonjwa sugu
- Vipimo vya maabara
- Huduma za kinga zinajumuisha ushauri nasaha, uchunguzi na chanjo
- Matibabu ya magonjwa sugu kama vile kisukari au pumu
- Matibabu ya watoto

## MFANO

Bima zote za afya zinapaswa kujumuisha mafao ya kulazwa hospitali. Wapigie *Washington Healthplanfinder* au kampuni ya bima yako kwa taarifa zaidi. Nambari yetu ni **1-855-923-4633**.

**Washington Health Benefit Exchange** inatii sheria zote husika za haki za kiraia za Serikali Kuu. Hatutabagua mtu kwa sababu ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu au jinsia.

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Cascade Care

## CASCADE CARE NI NINI?

Bima za afya zinazotoa mafao yale yale bila kujali ni kampuni gani ya bima unaichagua. Wana makato ya chini kuliko bima nyingi, na wanalipia huduma nyingi zaidi kabla ya kukidhi kigezo cha makato.

## CASCADE CARE SAVINGS NI NINI?

Programu ya Cascade Care Savings inashusha gharama ya ada yako ya bima ya afya. Ukiwa na ustahiki, jimbo litalipa sehemu ya ada yako ya bima.

Unaweza kustahiki Cascade Care Savings ikiwa mambo haya ni kweli:

- Kipato chako ni pungufu ya 250% ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu.
- Hustahiki Washington Apple Health (Medicaid) au Medicare.
- Una bima ya ngazi ya Fedha au Dhahabu ya Cascade Care.
- Ikiwa unastahiki punguzo la kodi, umekubali kiasi kamili unachoweza kupata.

## MFANO

Jen anataka kupata matibabu yake bila kukidhi kwanza kigezo cha makato. Kwa kuchagua bima ya Cascade Care kwenye *Washington Healthplanfinder*, Jen atapata mafao muhimu ya kiafya yanayolipiwa bila ile gharama ya awali.



MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI


# Kipindi cha Kujiandikisha

## KIPINDI CHA KUJIANDIKISHA NI NINI?

Ni kipindi cha mwaka ambapo unaweza kujiandikisha kwenye bima ya afya yenye ustahiki. Kinaanza Novemba 1 kila mwaka. Unaweza kutuma maombi Washington Apple Health wakati wowote.

## MFANO

Jackson anataka kujiandikisha kwenye bima ya afya. Anafungua akaunti kwenye **wahealthplanfinder.org** au app ya **WAPlanfinder**. Jackson anaweza kununua na kulinganisha bima za afya kuanzia Novemba 1 ili kujua iliyo sahihi kwake. Anajiandikisha kabla ya terehe ya mwisho. Bima yake ya afya itaanza Januari 1 ya mwaka unaofuata.




Tembelea **wahealthplanfinder.org** au pakua app ya **WAPlanfinder** ili ujiandikishe kwenye bima ya afya.

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Kipindi Maalum cha Kujiandikisha

## KIPINDI MAALUM CHA KUJIANDIKISHA NI NINI?

Baadhi ya matukio ya maisha yanakufanya ujiandikishe kwenye bima ya afya wakati wowote katika mwaka. Hiki kinaitwa kipindi maalum cha kujiandikisha. Tuma maombi ya kipindi maalum cha kujiandikisha hadi siku 60 baada ya tukio. *(Angalia mifano ya Tukio la Maisha lenye Ustahiki.)*

Ajira zinazotoa bima za afya lazima zitoe kipindi maalum cha kujiandikisha. Kipindi hiki kinadumu kwa siku 30.

## MFANO

Mke wa Mia amejifungua. Tukio hili linakuwezesha kuomba Kipindi maalum cha kujiandikisha. Anaingia kwenye akaunti yake ya *Washington Healthplanfinder* ndani ya siku 60 na kutuma maombi. Sasa anaweza kuchangua bima mpya inayojumuisha na mtoto.



Kujifungua na kuasili mtoto ni matukio ua maisha yenye ustahiki ambayo yanaweza kukuwezesha kubadilisha bima yako ya afya.

MANENO MUHIMU YA MWONGOZO WA MTUMIAJI

# Tukio la Maisha lenye Ustahiki

## TUKIO LA MAISHA LENYE USTAHIKI NI NINI?

Tukio la maisha lenye ustahiki linakuwezesha kujiandikisha kwenye bima ya afya wakati wowote katika mwaka. Inajumisha mabadiliko kama vile kuhama, ujauzito na badiliko la kipato. Una siku 60 tangu kutokea tukio kuomba kipindi maalum cha kujiandikisha. *(Angalia Kipindi Maalum cha Kujiandikisha kwa taarifa zaidi)*

## MIFANO YA MATUKIO YA MAISHA YENYE USTAHIKI

- Ndoa au kuishi kinyumba
- Kujifungua
- Kuasili au kulea watoto
- Kupokea amri ya mahakama (ikiwemo matunzo ya watoto)
- Kupoteza tegemezi au hali ya utegemezi kutokana na kifo, talaka au utengano halali kisheria.
- Badiliko la kipato
- Kupoteza bima nyingine ya afya
- Kuhamia Washington au kaunti mpya ya Washington
- Bailiko la uraia au hali ya ukazi halali kisheria
- Kuachiliwa huru kutoka gerezani
- Uanachama wa kikabila




Una siku 60 tangu kutokea tukio kuomba kipindi maalum cha kujiandikisha.

washington
healthplanfinder
click. compare. covered.

wahealthplanfinder.org
1-855-WAFINDER | 1-855-923-4633